**JIWE LA KUJENGEA LA KIROHO NO. 3**

# ILE SIRI YA MSALABA SASA IMEFUNULIWA

## *Ukristo ni kujikana mwenyewe.*

***Wagalatia 6:14 "lakini mimi hasha nisione fahari juu ya kitu chochote ila Msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo ambao kwa huo Ulimwengu umesulubishwa kwangu na mimi kwa Ulimwengu."***

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo sasa, kama tunataka kumuona yeye, kama umewahi kutegemea kumuona yeye, hutaweza kamwe kumuona yeye kwa kujiunga na Kanisa kwa kanuni fulani za sheria za vitabu. Unazojaribu kushika kwa maungamo fulani unayojaribu kutumikia. Utamuona Yeye utakapokufa, unapokuja Msalabani na unasulubiwa wewe mwenyewe, hapo sasa utaweza kumuona Yesu.

Unampata Yesu (Kristo) Msalabani pale unaposulubiwa pamoja naye. Huwezi kumpata kristo mpaka uwe umekuja wewe mwenyewe na kumkubali Yeye, lile neno, hapo sasa unapata uzima.

Mwanafunzi halisi atakuleta moja kwa moja katika uwepo wa Kristo, na kutoka hapo Kristo atakuonyesha yakupasayo kutenda. ***(Yohana 12:20-26)***

Lakini Kristo aliwaleta wao msalabani na ukimpata mwanafunzi halisi Yeye atakuelekeza kwake Kristo, Kristo atakuelekeza msalabani ambapo usulubiwe pamoja naye. ***(Rumi 6:6)*** na uzima wake wa milele unakutana na uzima wako. Na uzima wako unakufa unachukua uzima wake wa milele hapo sasa unakuwa mwana wa Mungu Amina. Kuna tofauti sana kati ya wanafunzi wa zamani na wanafunzi wa leo.

Kristo mwenyewe aliwaelekeza watu kwenye kifo chake na akasema, "Amini amini nawaambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi ikafa hukaa hali hiyo hiyo peke yake, bali ikifa hutoa mazao mengi ***(Yohana 12:24)***

Nitawaelekeza ninyi mahali ambapo mimi nitaenda kusulubiwa kwa ajili yenu, na ndani pale kama mtasulubiwa pamoja na mimi, utatambua mimi ni nani ***(Mathayo 16:24-25)***

Oh! jinsi ilivyo tofauti! ndiyo Bwana. Jinsi ilivyo tofauti. Lakini maisha yako na maisha yake yakutane yote pale, siyo katika kanisa, siyo katika jengo, siyo katika kanuni, siyo katika matendo, lakini ni pale msalabani ambapo unasulubiwa pamoja naye ***(Wagalatia 6:14)***

Hapo ndipo unampata Kristo, humpati Yeye katika kufanya vizuri, kwa kufungua ukurasa mpya, kuanza maisha mapya, huko hutaweza kumpata Kristo, Unampata Kristo tuu katika Mauti, sio katika holi la ng'ombe, sio katika ungamo. Kuamini kanuni fulani na mambo ya uongo, humpati Kristo hapo, Mtumishi wa kweli huchukuwa kwake , na Yeye ni Neno.

Unasema “Sasa ndugu Branham kama Kristo yuko Duniani leo, Mtumishi halisi atamchukuwa kwake, Ukristo” Vema, Kristo yupo hapa katika umbo la neno; na lile neno linaleta uhai, kwa sababu yeye ni neno ***(Yohana 6:63)*** Kristo ni Neno. Ndiyo, Bwana. Yeye mwenyewe ni neno. Mtumishi wa kweli atakuleta kwenye neno.

Sasa, yeye ni neno. Yeye ni hii biblia inakuwa hai au ni hii biblia inaishi. Na wakati unakufa wewe mwenyewe pamoja na Kristo kama mbegu ya ngano, hapo sasa lile neno linaishi ndani yako likileta matokeo yale yale kama ilivyofanya kwenye mbegu ya ngano ambayo ilibidi ianguke chini katika udongo (Duniani) Amen. Ninyi ni washirika katika kufufuka kwake. Ninyi ni washirika wake katika Baraka zake zote, katika madhihirisho yake yote. Ninyi ni washirika wake katika yote aliyoyafanya. [1]

Sasa kama wewe ni mwana wa binti wa Mungu, hapo inamaanisha ulikuwa ndani ya Mungu tangu mwanzo. Wewe ni sifa zake, kama hukuwepo pale wakati huo ina maana kamwe hukuwepo au kamwe hautakuwepo ***(Yohana 17:6,9-16)***

Wana wa binti za Mungu walikuwepo ndani yake tangu mwanzo sasa angalia, unao uzima wa milele, unasema, Unasema. Tunaamini hilo kuwa tunao uzima wa milele ***(Yohana 5:24)*** Vema, kuna aina moja tu ya uzima wa milele, na hiyo ni Mungu. Hicho ndicho kitu pekee ambacho ni cha milele, ni Mungu hapo sasa kama una uzima wa milele, uzima huo ulikuwa ndani yako, na ulikuwa katika viuno vya Mungu kabla haijakuwepo Dunia. ***(Waefeso 1:3-5)*** Yesu mwenyewe anaitwa Neno, Na katika Yohana mt. 1 alisema “ Hapo mwanzo kulikuwako Neno, na Neno alikuwa kwa Mungu, na Neno alikuwa Mungu, na Neno akafanyika mwili akakaa kwetu”

***(Yohana 1:1-2, 14-18)*** Hapo ulikuwa katika viuno vya Yesu, na ulienda msalabani pamoja naye, ulikufa pamoja naye nawe ukafufuka pamoja naye. na leo tumeketi pamoja naye. Katika mazingira ya Kimbinguni (Ulimwengu watosha) ***(waefeso 2:6-7)*** Tukiwa tumejazwa na roho wake, wana wa binti wa Mungu. Kufa pamoja naye kufufuka pamoja naye! Hakika [2]

Katika kuwaza kwake Mungu mwenyewe, Yule Roho mkuu, pale mwanzo kabla hapajawa na mwanzo. Yeye alikuwa Mungu na mlijua mlikuwa ndani yake wakati huo?

Na sasa kama hiyo iko hivyo, ule Uungu wote uliumbika katika utu wa Yesu kristo kimwili ***(Kolosai 2:9-10)*** na hapo sasa Yesu Kristo alipokufa pale msalabani, nilikufa pamoja naye, kwa maana wakati huo nilikuwa ndani yake, kwa maana alikuwa ukamilifu wa Neno likithibitishwa ikijulikana kuwa tutakuja dhihirishwa baadae. Nasi tulikuwa pale msalabani pamoja naye, Tulienda kaburini pamoja naye, nasi tulifufuka pamoja naye katika ufufuo wake ***(Rumi 6:3-5)*** na sasa tumepaa kwa Roho wake, kwenye kiti cha rehema, tukiwa tumekaa pamoja katika mazingira ya kimbinguni ndani ya Yesu kristo siku zote.

Kwa maana kama vile chembe ya uhai wa asili inayoletwa chini, ilirutubishwa kutoka Baba kwenda Baba, Ndivyo hivyo hivyo uhai wa kristo unavyorutubishwa. Hiyo ndiyo sababu Mungu anaitumia Roho ya Eliya mara tano tofauti. Hiyo ni nini? ni kule kuendeleza hiyo katika vizazi.

Kama vile maisha yako ya kimwili na tabia zinavyorithishwa kutoka kwa ule uzalishaji wa baba yako, kadhalika Roho wa Mungu, ambaye alikusudiwa kuibeba kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na wakati neno lote la Mungu lilipokusanywa lote kwa ukamilifu katika mwili wa kibinadamu uitwao Yesu Kristo, Ndani pale Mungu alinifanya nilipie dhambi zangu, ndani yake pale. Hapo akanifufua mimi pamoja naye, katika kule kufufuka, na sasa tumeketi pamoja naye, tukiwa na nguvu na uwezo/ mamlaka juu ya kila pepo ***(waefeso 1:15-23)*** Oh kama tuu mnaweza kuamini kile Mungu alichotupa, kutenda, kamwe hautaitumia. Lakini kama umeketi pale, utaitumia kwa maana ukikusudiwa ufanye kile unachofanya. [3]

Basi kumbuka pale ulipokuwa katika viuno vya Baba yako, ulikuwa naye wakati huo. Lakini Baba yako hakukujua wewe wakati huo. Nawe hukumjua Baba yako na ilibidi uje uzaliwe . Mungu alifanya njia kupitia mama kwa ajili ya mahali pa kukalia mbegu, nayo ikaja nawe umekuwa mwanaume au mwanamke, chochote kile kiwacho hapo ulimtambua baba yako, na baba yako angeweza kuwa na ushirika nawe.

Sasa kumbuka kama una uzima wa milele, uhai wako ulikuwa ndani ya Mungu tangu mwanzo. Na ule uhai. Mungu ni Neno halafu lile neno likafanyika mwili katika Yesu Kristo. Mungu alikuja chini kukaa katika mwili wake mwenyewe ***(Wafilipi 2:5-8)*** amejifanya/ kujiumba mwenyewe mwana wa Mungu. Mungu alipokuja kukaa katika huo, ulikuwa ndani yake, naye pale aliposulubiwa na wewe ulisulubiwa pamoja naye, nawe ulikufa pamoja naye pale msalabani ulizikwa pamoja naye. Pale mlimani, Nawe ulifufuka pamoja naye ile asubuhi ya pasaka. Na sasa mmekaa pamoja katika ulimwengu wa kiroho ndani yake. Na sasa mnao ushirika pamoja naye unaona?

Mungu mwenyewe amekuwa mmoja wetu, hakuna aliye mwona baba, wakati wowote mwana pekee wa baba ndiye amemdhihirisha yeye ***(Yohana 1:14-18)*** hiyo ni Mungu amefanyika kuwa mtu, ili aweze kuwa na ushirika na wewe kama mtu ***(1Timotheo 3:160)*** unaona? Na sasa wewe ni mwili wa nyama na Yeye ni mwili.Mungu amefanyika mwili miongoni mwetu katika utu wa mwana wake Yesu kristo. Na ndani yake kulikuwa ni Mungu, hakupungukiwa chochote cha Mungu, alikuwa Mungu "Mungu alidhiririshwa katika mwana . Yesu Kristo" ambalo limemfanya kuwa Emmanuel, kama Nabii alivyosema angekuwa hivyo. ***(Mathayo 1:21-23)*** [4]

Lazima ije … Sawa na vile Yesu alivyokuja kwa kujitoa mwenyewe kuwa sadaka/dhabihu kutoa vyote vilivyo vyako kwa Mungu. Na kutembea kuelekea msalabani na kusulubiwa pamoja naye kuinuka/ kufufuka tena, kuvaa mavazi yake ya sadaka. Dhabihu – na mauti kwa mambo ya Dunia. [5]

Na mwaminio anayekuja kwa Yesu lazima aje kwenye msalaba wa kujikana mwenyewe ***(Luka 9:23)*** na kufa pale na Mwanakondoo wako, pamoja na Mwanakondoo wake. Afe mwenyewe kwa mawazo yake, ufe mwenyewe kwa uwezo wako wa kiakili wa kuwaza! uchukue tu kile Roho Mtakatifu anachosema moyoni mwako. Na hapo sasa uishi kwa ajili ya Kristo. [6]

Marafiki sipendi kusema hili kama mkosoaji, lakini tumeshindwa kutenda sawa na utaratibu ambao Kristo ametutuma sisi kufanya. Unaona? Amesema “Enendeni ulimwenguni mkaihubiri injili” hakusema mkajenge shule, hakusema mkajenge makanisa na madhehebu ambavyo vimefanya sehemu yao, lakini hivyo sivyo alivyosema “Hubiri injili, na ishara hizi zitafuatana nao waaminio” kwa maneno mengine, kuhubiri injili kungekuwa ni kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu ***(Marko 16:15-18)*** na hapo ndipo tuliposhindwa.

Lile kanisa linachohitaji leo, sio kitu laini cha haibreed, laini na legevu, kama kanisa lilivyo leo kule kufanya ungamo tuu, na kubatizwa na hapo umekuwa Mkristo ni kujikana mwenyewe “ Jikane mwenyewe na uchukue msalaba wako kila siku na unifuate mimi” ***(Luka 14:25-35).*** Leo ni laini sana na watu wanajiita wenyewe ni wakristo, kuna wakati ilimaanisha kufa, unapomkiri Kristo. Na ilibidi umtegemee Yesu kila siku kwa chochote utakachokihitaji. [7]

Na ni mchanganyiko wa namna gani ambao wakristo wameingia leo. Wanafikiri kwamba Ukristo ni kitu laini sana. Wafanyavyo wote ni kuwekea jina katika kitabu, na kumpata mtu ambaye atawanyunyizia maji au kitu kingine na kumpa mhudumu mkono wa kuume wa ushirika na hilo ndilo tu la kufanya! Na kuendelea mbele. Huu sio Ukristo.

Ukristo ni kujikana mwenyewe ***(Luka 9:23)*** kuchukua msalaba wako kila siku! Na kumfuata Yeye! ***(Mathayo 16:24-25).*** Ufe kabisa, kwenye mambo ya ulimwengu! Mahali ambapo hukumu yetu imeondoka, “Sasa, basi hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio ndani ya Kristo Yesu? ***(Warumi 8:1-2)*** unaingiaje ndani yake? Kwa kujiunga? Hapana. Kwa kupeana mikono? Hapana. Kwa kuungama?, kwa elimu? Kwa roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika mwili mmoja ***“(1Kor 12:13)*** kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu tunakuwa ndani ya Kristo” Na hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio ndani ya Kristo Yesu, ambao hawatembei kwa kuufuata mwili, bali hufuata Roho. Amina. Oh hilo, hilo litamfanya yoyote yule apige makelele amina. [8]

**Nukuu za Kiingereza**

[1] “Mabwana tunataka Kumuona Yesu” (61-1224) uk. 15, 17, 22.

[2] Nguvu za mungu za kubadilisha” (65-0911), aya 232-234.

[3]”Munu wa wakati huu muovu”(65-0801M), Aya 67-69.

[4]” Kiu” (65-0919), Aya 194-196.

[5]”Mambo yatakayokuwa”(65-1205), Aya 109-110.

[6]”Kristo”(55-0221), Aya E.17

[7]” Mkuu zaidi ya Suleimani Yuko hapa”(63-0605)Aya 37-38.

[8]”Usiogope”(63-0607), Aya 105-106

---

Jiwe la kiroho la kujengea No. 3 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69, D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax (+49)72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka Dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*